# *BARUA #04; NAMBA, NJIA PEKEE YA KUJIPIMA.*

Karibu sana rafiki yangu mpendwa kwenye barua yetu nyingine kwenye mwaka huu wa mafanikio 2020/2021.

Kwenye barua ya leo nakwenda kukushirikisha namna pekee ya kujipima kwenye safari yetu ya mafanikio makubwa ambayo tunakwenda pamoja.

Kwenye tathmini zetu za kila mwezi, swali namba nne linauliza utaje namba unazojipima nazo kila mwezi na kushirikisha jinsi ulivyofikia namba hizo.

Ni swali ambalo baadhi ya wanamafanikio wameeleza kwamba hawalielewi na hawajui jinsi gani ya kujipima kwa namba.

Hivyo barua ya leo itakwenda kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu namba na jinsi ya kuzitumia kujipima na kujisukuma na pia utaweza

kujiwekea namba sahihi utakazokuwa unafanyia kazi kila siku.

## Tatizo la malengo.

Malengo yamekuwa yanalaumiwa sana, kila siku ya mwaka mpya watu wengi hujiwekea malengo mbalimbali kwa mwaka husika.

Wengi utawasikia wakisema mwaka mpya mambo mapya, au mwaka huu nitaanza biashara, nitajenga, nitanunua gari, nitaoa/kuolewa na mengine mengi.

Hiyo ni siku ya tarehe moja Januari. Mfuate mtu huyo huyo tarehe moja Februari na atakuwa anaongelea mambo hayo kwa mbali mno. Rudi kwake tarehe moja Machi na atakushangaa, hatakuwa tena anaimba malengo hayo aliyojiwekea siku ya mwaka mpya.

Pamoja na lawama zote kwenda kwenye malengo ya mwaka mpya kwamba mengi hayafikiwi, malengo hayana tatizo, bali matatizo yako kwetu ambao tunayaweka malengo hayo.

Kwa walio wengi, huwa wanaweka malengo yaliyo wazi na yasiyopimika. Kwa kuwa na malengo ya aina hiyo, hakuna kinachomsukuma mtu na hivyo hawezi kubaki kwenye hayo malengo.

Malengo yasiyokuwa na namba ya kuyapima, huwezi kuyafikia na hata ukiyafikia, huwezi kujua kama umeyafikia. Hivyo hitaji moja kubwa na la msingi kwenye malengo yoyote ambayo mtu unajiwekea, ni kuwa na namba unayojipima nayo kama unayafikia au la.

## Kliniki ya watoto.

Kwa wengi wetu tayari tuna watoto na hata kama huna wa kwako, umeishi kwenye familia yenye watoto wachanga.

Unajua fika kwamba mtoto anapozaliwa, kwa angalau miaka miwili ya kwanza, kila mwezi anahudhuria kliniki.

Huko kliniki anakopelekwa, pamoja na mambo mengine ya kiafya, anapimwa maendeleo yake, kwa uzito na urefu.

Hizi ni namba muhimu mno kwenye kupima ukuaji wa mtoto. Kwa kulinganisha na ukuaji wa kawaida, mtoto anafuatiliwa kuonekana kama anakwenda sawa na umri wake au siyo sawa.

Kama uzito wa mtoto uko chini kuliko kawaida, wazazi watashauriwa njia bora ya kumlea mtoto hasa kwenye lishe ili aweze kwenda sawa kwenye uzito.

Bila ya kwenda kliniki na kuzijua namba hizo kuhusu mtoto, mzazi hawezi kujua maendeleo ya mtoto wake. Hivyo hata kama mzazi ametingwa kiasi gani, atahakikisha kila mwezi anahudhuria kliniki ya mtoto wake.

Jionee hapo rafiki yangu, jinsi ilivyo muhimu kuwa na namba kwenye ukuaji wa mtoto au kitu kingine chochote. Lakini wengi hawajiwekei namba kwenye ukuaji wao binafsi na kufikia mafanikio makubwa.

## Kujipima kwa namba.

Namba ndiyo njia pekee ya kupima vitu. Kabla ya kuja kwa vipimo vya namba, haikuwa rahisi

kupima vitu na hivyo watu hawakuweza kujua vitu kwa uhakika. Lakini tangu kugunduliwa kwa namba, imekuwa njia sahihi ya kufikia makubaliano baina ya watu.

Bila ya kuwa na namba kuhusu kitu, ni vigumu kufanya maamuzi juu ya kitu hicho.

Kukosekana kwa namba kumekuwa njia ya baadhi ya watu kujificha na kuwalaghai wengine. Chukua mfano wa mtu anayeenda kijijini kununua mazao, akifika huko ananunua kwa furushi la kukadiriwa, ila akifika mjini anaenda kuuza kwa kilo.

Kule kijijini kwa sababu watu hawajui umuhimu wa namba au hawajui bei ya mazao yao kwa namba, wanakuwa tayari kuuza kwa bei yoyote watakayopewa na kuona inawatosha.

Sasa achana na hao wanaodanganywa na wasio waaminifu, rudi kwako mwenyewe. Kwa kukosa namba za kujipima, umekuwa unajidanganya. Unajiwekea malengo na mipango, ambayo huna namba za kujipima na muda ukiisha

unaweza kujitangazia umeshinda au imeshindikana hata kama siyo kweli.

Kwa sababu huna namba, chochote kitakubalika kwako. Kama unajiambia lengo ni kuwa na fedha nyingi, kama sasa una laki moja, laki moja na elfu kumi ni nyingi kuliko laki moja, hivyo tayari hiyo ni fedha nyingi.

## Weka namba.

Kwa malengo na mipango yoyote unayojiwekea kwenye maisha yako, hakikisha una namba za kujipima kama unayafikia au la. Bila namba, hesabu huna malengo wala mpango wowote na unajifurahisha tu.

Kuna aina mbili za namba za kujiwekea kwenye malengo na mipango yako.

Aina ya kwanza ni namba ya kiwango, wingi au ukubwa, hapa unapima kile kiwango unachotaka kufikia, kama ni fedha unaeleza kabisa kiasi, kama ni eneo unaeleza ukubwa. Hii ni namba muhimu inayokuwezesha kupima na

kujua kama unakwenda sawa na kama umefikia au la.

Aina ya pili ni namba ya muda, hapa ni muda unaokuwa umejipa wa kufikia lengo husika. Bila ya kuwa na muda, hutasukumwa kuchukua hatua, utaona muda bado upo, ila unapojiwekea ukomo wa muda kwenye chochote unachofanya, unalazimika kuchukua hatua ili ukamilishe ndani ya muda.

Hivyo kitu chochote unachofanya, jua unataka kufika wapi na kwa muda gani. Bila namba hizo mbili, hutaweza kupiga hatua kwenye yale unayofanya.

## Jinsi ya kukokotoa namba zako.

Baada ya kujua umuhimu wa kuwa na namba za kujipima kwenye safari ya mafanikio, kinachofuata ni kujua jinsi ya kukokotoa namba zako.

Hii siyo hesabu ngumu, wala huhitaji kuwa unajua hisabati sana ndiyo uweze kufanya hivyo.

Unachohitaji kujua ni wapi unataka kufika na unataka ufike hapo lini. Ukishajua hayo, sasa unakaa chini na kukokotoa hatua za kupiga ili uweze kufika hapo kwa muda huo.

Chukua mfano umejiambia unataka kufikia uhuru wa kifedha mwaka 2030. Kwanza hili siyo lengo sahihi na hata ukeshe unajitesa, huwezi kulifikia. Japo una namba kwenye muda, huna namba kwenye kiwango, hivyo ni vigumu kufikia kitu usichokijua.

Uhuru wa kifedha ni dhana pana, usipoweka namba, itakuwa vigumu mno kufikia.

Hivyo tukirudi kwenye lengo la uhuru wa kifedha, unapaswa kujipa namba.

Kwanza kabisa anza na maana ya uhuru wa kifedha, ambayo ni maisha yako kuweza kwenda vizuri hata kama hufanyi kazi ya kukuingizia kipato. Maana yake unakuwa na akiba na uwekezaji ambao unakuwezesha kuendesha maisha yako bila ya kuwa na wasiwasi.

Baada ya kujua maana hii, unahitaji kujua gharama za kuendesha maisha yako ni kiasi gani kwa mwaka, kwa wastani. Unaweza kukokotoa kwa sasa kama hakuna mabadiliko makubwa unayotaka kufanya au kukadiria kwa baadaye kulingana na viwango unavyotaka kufikia.

Baada ya kujua kiwango cha kuendesha maisha yako kwa mwaka, chukua namba 100 (makadirio ya miaka utakayoishi, haya ni makadirio ya juu kulingana na viwango vya miaka ya kuishi) na toa miaka utakayokuwa nayo kufikia mwaka huo 2030. Kwa mfano kama mwaka 2030 utakuwa na miaka 45 ina maana 100 – 45 ni 55. 55 ndiyo namba yako ya kufanyia kazi, kwamba kufika mwaka 2030 uweze kuwa na akiba na uwekezaji ambao unaweza kuendesha maisha yako kwa miaka 55 bila ya wewe kufanya shughuli ya kuingiza kipato.

Kama njia hiyo ni ndefu, unaweza kuchagua namba ambayo ni kubwa, ambayo itaweza kuendana na maisha yako kwa kipindi chochote kitakachokuwa kimesalia.

Mfano wa namba hiyo ni dola bilioni moja na kuendelea. Kwa kufikia kiwango kama hicho, una uhakika wa kuyaendesha maisha yako yote vizuri hata kama hutafanya kazi. Lakini hapa kuna tahadhari nyingine, kuepuka kufanya mambo ambayo yatapoteza kiasi hicho cha fedha ulichokipata.

Baada ya kujua namba yako kwa miaka 10 ijayo, unaigawa kwa kila mwaka kujua unapaswa kuweka akiba na kuwekeza kiasi gani ili kufikia lengo. Miaka ya mwanzo utaanza kidogo, lakini kadiri unavyokwenda, uwekezaji ambao umeanza kuufanya unaendelea kukua.

Ukishakuwa na namba ya mwaka, unaweza kuigawa kwenye mwezi ili kuweza kujua unapaswa kufanya nini kila mwezi. Hapo pia unaweza kuendelea kuigawa kwenye wiki na hata siku. Kadiri namba yako inavyokuwa imegawanywa kwenye muda mfupi, ndivyo inavyokuwa rahisi kujipima na kujisukuma.

Mfano ukijiwekea lengo la kifedha la mwaka, itakuchukua mwaka mzima kuja kujitathmini

kama umefikia, na kama mwaka utaisha na ukagundua hujafikia, huna cha kufanya, inabidi uanze upya mwaka unaofuata.

Lakini kama umejiwekea lengo la mwezi, kisha mwezi ukaisha na hujafikia, ni rahisi kujisahihisha kwenye mwezi unaofuatia.

Ndiyo maana kwenye tathmini zetu za kila mwezi, tuna swali hilo la namba unazojipima nazo na matokeo yake, kwa kujua kwenye mwezi mmoja, utasukumwa kuchukua hatua mwezi unaofuata ili namba ziwe bora zaidi.

## Namba muhimu kwenye safari ya mafanikio.

Kwenye safari hii ya mafanikio ambayo tupo pamoja, ambapo kwa sasa tupo kwenye MUONGO WA KUFANYA MAKUBWA 2020-2030 tunapaswa kuwa na namba ambazo kila mmoja wetu anajipima nazo.

Hapa nimeweka makundi muhimu na namba za kujipima nazo.

1. Ukuaji binafsi; hapa unahitaji kuwa na namba ya vitabu unavyosoma na mabadiliko binafsi kwenye maisha yako, kuacha tabia zilizo mbaya na kujenga tabia zilizo nzuri kwa mafanikio yako. Hivyo weka namba ya vitabu utakavyosoma kwa mwaka kisha gawa kwenye mwezi. Pia orodhesha tabia zote zinazokukwamisha na chagua zile ambazo utavunja kwenye mwaka na hatua unazochukua kila mwezi. Mwisho chagua tabia mpya za kujijengea ili uweze kufanikiwa na zijue pamoja na hatua za kuchukua kila mwezi kujenga tabia hizo.

2. Fedha; hapa jipe namba ya kipato unachotaka kuingiza, akiba unayopanga kuweka na uwekezaji unaopanga kufanya. Kuanzia hiyo miaka kumi, kisha mwaka na hatimaye mwezi. Kisha kila mwezi jipime kwa jumla ya kipato ulichoingiza, akiba uliyoweka na uwekezaji uliofanya. Kama ni chini ya lengo basi jisukume mwezi unaofuata kufikia lengo.

3. Afya; hapa unahitaji namba za kujipima kwenye malengo na mipango ya kiafya, mfano

kwenye uzito wa mwili, muda unaofanya mazoezi, kiwango cha chakula na muda unaopumzika. Jipe namba unazopaswa kufikia, kwa uzito usizidi ngapi (hapa tafuta BMI yako na kisha jua uzito ambao hupaswi kuupitiliza), idadi ya muda wa mazoezi, kwa wiki (mfano dakika au masaa ya mazoezi) na muda unaopumzika (mfano masaa unayolala na yale unayokuwa peke yako). Afya inajengwa au kubomolewa na vitu vitatu, unachokula, mazoezi na kupumzika, hivyo ukijipa namba kwenye hayo na kuzifanyia kazi, utakwenda vizuri kiafya.

3. Mahusiano; hapa jipe namba ya muda unaotenga kwa ajili ya wale muhimu kwako.

4. Kazi; hapa jipe namba ya masaa unayoweka kwenye kazi na matokeo unayozalisha. Kila siku lenga kuwa na masaa fulani ambayo unafanya kazi bila ya usumbufu. Na pia kuwa na kiwango cha kazi unazopanga kuzalisha kila siku, wiki au mwezi. Mfano kama unaandika, basi jipe namba ya maneno kwa siku, wiki na mwezi. Kama ni vitu unazalisha basi jipe namba ya kiasi

utakachozalisha. Kama ni huduma unatoa, jipe namba ya idadi ya utakaowahudumia. Kwa kazi yoyote unayofanya, kuwa na namba ya masaa unayofanya na kiwango unachotaka kuzalisha ili kufikia lengo la mwaka na la muongo.

5. Biashara; hapa kuna namba nyingi za kupima, lakini kwa msingi kabisa, kila anayefanya biashara anapaswa kujipima kwa namba hizi tano; mtaji unaozunguka, mauzo, gharama za kuendesha biashara, idadi ya wateja na faida kamili iliyopatikana. Lazima uwe na namba unazotaka kufikia kwenye maeneo hayo matano na kisha kila mwezi kujipima umefanya kwa kiwango gani. Unapojua namba ya mwezi unaomaliza, unapanga kujisukuma zaidi kwenye mwezi unaofuata.

6. Mengineyo; kuna mengine ambayo hayaingii kwenye aina hizo tano, lakini umepanga kuyafanya au kuyafikia. Chochote kile, kipe namba na kisha jipime kwa namba hizo. Iwe ni kwenye kilimo, uwekezaji au kingine chochote, jipe namba unayotaka kufikia ndani ya miaka

10, gawa kwa mwaka kisha kwa mwezi halafu kila mwezi jifanyie tathmini.

## Mipango siyo matumizi.

Hakuna ambaye huwa hapangi, lakini ni wachache mno wanaoendelea na mipango yao.

Hiyo ni kwa sababu wewe unapanga yako vizuri sana, lakini uhalisia unakuja kuwa tofauti kabisa na mipango yako.

Umejipangia kila mwezi uingize kipato cha milioni 5, umepambana kweli kwa kila namna unayoweza, umeishia kuingiza milioni 1. Hapo ndipo wengi hukata tamaa na kuona kupanga ni kupoteza muda.

Ukweli unaopaswa kuujua na kwenda nao ni huu; MIPANGO SIYO MATUMIZI, siyo kila unachopanga kitaenda kama ulivyopanga. Lakini kupanga ni lazima, kwani usipopanga kabisa, maana yake unakuwa umepanga kushindwa.

Kadiri unavyofanyia kazi mipango yako, kuna mambo utajifunza ambayo hukuwa unayajua

wakati unaweka mipango yako. Hivyo badala ya kukata tamaa, unapaswa kuboresha mpango wako ili uweze kuendana na uhalisia.

Hivyo mpango wowote unaojiweka kwenye namba, siyo kwamba utazifikia kama ulivyoweka, ila utakuweka kwenye njia sahihi na hapo utazidi kuboresha mpaka kuweza kufika kule unakotaka kufika.

Kingine muhimu kujua ni kwamba hutapatia kwenye yote unayopanga, kuna mengi utashindwa, lakini machache utakayokuja kushinda, yatalipa yote uliyopotea.

Hivyo usiache kabisa kupanga kwa sababu matokeo unayopata hayaendani na mipango yake. Bali kaa chini na boresha mipango yako au hatua unazochukua mpaka uweze kufika kule unakotaka kufika.

Mafanikio makubwa siyo rahisi, ndiyo maana siyo wengi waliofanikiwa, lakini pale unapodhamiria kweli, unapojua nini hasa unataka na wapi unataka kufika, kisha ukawa na namba za kupima kama umefika na

ukajitathmini kwa namba hizo kila mwezi, utalazimika kukaa kwenye njia sahihi na kuacha kuzurura.

## Hatua za kuchukua kwenye tathmini za kila mwezi.

Naamini kila mmoja wetu amepata ufafanuzi wa kina kuhusu namba za kujipima kwenye safari ya mafanikio.

Sasa kila mmoja wetu akae chini na kuiangalia ndoto yake kubwa na mpango wa muongo kama alivyonishirikisha. Kisha kujipa namna kwenye mpango wa muongo, kugawa kwa mwaka na kisha kugawa kila mwezi.

Fanya zoezi hilo pia kwenye maeneo mengine ya maisha yako unayotaka kupiga hatua.

Kisha kuwa na namba zako unazojipima nazo kila mwezi na kwenye tathmini ya kila mwezi, shirikisha namba unazojipima nazo na matokeo uliyopata kwenye mwezi husika.

Mfano wa jinsi ya kutuma kwenye tathmini;

Namba ninazojipima nazo na matokeo niliyopata kwa mwezi .....

Vitabu vya kusoma - 4, nilivyosoma - 3

Jumla ya kipato – Tsh 5M, nilichoingiza – 2M

Akiba ya kuweka – Tsh 1M, niliyoweka – 300K

Kadhalika kwa namba nyingine unazofanyia kazi, kila mwezi ziripoti hivyo.

Kisha kwa namba ambazo umekwenda chini ya lengo, jiulize nini kimepelekea ushindwe kufikia lengo na angalia wapi pa kuboresha ili upate namna nzuri zaidi mwezi unaofuata.

Usiendelee mwezi kwa mazoea ya mwezi uliopita, kila mwezi lazima uwe na mkakati mpya unaofanyia kazi wa kukuza zaidi namba zako.

Mfano kama namna ya wateja unayojipima nayo kwenye biashara ni 100 kwa mwezi, lakini umeweza kuhudumia wateja 60 tu, usiendelee kufanya kile ulichofanya ukapata wateja 60, lazima uwe na mkakati mpya wa kukuwezesha kuhudumia wateja zaidi ya hao.

MUHIMU; Kwenye biashara yako, kila mwezi tuma tathmini ya namba 5 kwa mpango wako na kwa matokeo uliyopata.

# MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021